SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu vya 6(1) (q), 7(1) na 16(l)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA

YA RUANGWA, 2O15

SEHEMUYA KWANZA
UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa za (Ada na Ushuru) za Mwaka 2015 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa. Sheria Ndogo hizi zitafuta Sheria ndogo za Ada na Ushuru za Mwaka 2008, ziliyotangazwa kwa Tangazo la Serikali namba 273 la tarehe 14/08/2009.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

"Ada na Ushuru" maana yake ni ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa Mipango Miji; Mhandisi wa Ujenzi au Afisa yeyote na inaweza kujumuisha wakala aliyeidhinishwa au kuteuliwa kusimamia Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.

"Mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu na. l4 ya Mwaka 2002 chini ya kifungu no. 2 ni kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na mazao ya miti yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao; mbegu za miti, nta, asali, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani ya mizizi, gundi, utomvu, maranda,

matete, kamba, makuti (mawale); nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kilichotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la misitu.

"Madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, kokoto, na mawe yanayochimbwa katika eneo la Halmashauri.

"Minara" maana yake ni minara yote itakayowekwa kwa ajili ya mawasiliano ya simu, fax, radio yenye urefu unaozidi mita ishirini (20).

"Mkurugenzi"maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Ruangwa pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mnunuzi" maana yake ni mtu yeyote kikundi cha watu, kampuni au taasisi yenye kununua mazao ya kilimo au misitu ndani ya eneo la Halmashauri.

"Nyumba ya wageni" maana yake ni nyumba iliyoandaliwa nakufuata masharti ya kibiashara kwa madhumuni ya kuwapokea wageni au wasafiri kwa nia ya kupata faida, lakini haitajumuisha;-

a) Mahali palipoandaliwa kwa ajili ya wageni wasiozidi sita (6),
b) Mahali palipoandaliwa mabweni kwa ajili ya malazi,
c) Nyumba za serikali zinazotoa huduma za malazi au
d) Nyumba zilizoandaliwa kwa ajili ya watalii na kuandikishwa chini ya Sheria ya Utalii.

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290

"Vibao vya matangazo" maana yake ni vibao vyenye maandishi vilivyobadikwa mbele ya vibanda vya biashara kwa lengo Ia kutangaza au kuvumisha biashara.

"Vyombo vya usafiri vya kibiashara" maana yake ni vyombo vyote vinavyotoa huduma ya usafiri ambapo itajumuisha aina zote za magari, pikipiki za gurudumu mbili na gurudumu tatu.

Ada na Ushuru

4. (1) Kutakuwa na ada na ushuru utakaotozwa na kukusanywa kwa ajili ya huduma mbalimbali, vibali na leseni zitolewazo na Halmashauri kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utatakiwa kulipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Halmashauri itatoa stakabadhi yenye nembo ya Halmashauri kwa ajiri ya malipo ya Ada na Ushuru uliolipwa.

SEHEMU YA PILI
ADA YA VIBALI VYA UJENZI

Usimamizi wa Ada na maombi ya Viwanja

6. (1) Halmashauri itatoza Ada kwa ajili ya vibali vya ujenzi kwa viwango vinavyooneshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi kulingana na maeneo ambayo kibali hicho kinaombwa.

(2) Maombi ya kibali cha ujenzi yatawasilishwa pamoja na ramani ya ujenzi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga katika maeneo ya mji bila kuwa na kibali kutoka Halmashauri.

(4) Afisa muidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kufanya ukaguzi.

SEHEMU YA TATU
USHURU WA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

7 (1) Kila mnyama aliyechinjwa kwenye machinjio ndani ya eneo la Halmashauri isipokuwa maeneo ya vijijini atalipiwa ushuru wa ukaguzi wa nyama na ushuru wa machinjio kwa viwango kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (1) cha kifungu cha 7 hapo juu, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kutoza ushuru wa ukaguzi wa nyama kwa wanyama wachinjwao vijijini ikiwa nyama hiyo itakuwa ni kwa matumizi ya watu wengi.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mnyama kwa ajili ya matumizi ya watu wengi kabla ya kukaguliwa kama anafaa kwa matumizi ya binadamu.

SEHEMU YA NNE
ADA ZA MALI ZA HALMASHAURI

Wapangaji kulipa pango

8. (1) Kila mpangaji kwenye nyumba au kibanda kinachomilikiwa na Halmashauri atatakiwa kulipa kodi ya pango ya nyumba au kibanda kwa viwango kama vilivyooneshwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Wapangaji kuingia mkataba

(2) Isipokuwa kwa watumishi wa Halmashauri wapangaji wa nyumba za Halmashauri watatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri

kabla ya kuingia kwenye nyumba hizo.

(3) Halmashauri itaweka utaratibu wa umiliki wa vibanda sokoni au sehemu nyingine yoyote iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vibanda hivyo kwa kusaini mikataba.

(4) Kibanda au Kizimba chochote ambacho kitakuwa hakijafunguliwa na kulipiwa kodi ya pango kwa muda wa miezi sita bila sababu kitachukuliwa na Halmashauri na kugawiwa kwa mtu mwingine na mmiliki wa awali ataendelea kudaiwa malimbikizo ya kodi.

SEHEMU YA TANO
USHURU WA MAZAO YA MISITU

GN No. 33/2015

9. (1) Halmashauri inaanzisha na kutoza ushuru wa mazao ya misitu, kwa mazao yote yatakayovunwa ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Ushuru huo utatozwa kutoka kwa kila mnunuzi wa mazao ya misitu kwa kiwango cha asilimia tano ya bei ya kununulia kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(3) Mnunuzi yeyote anayetaka kununua mazao ya misitu katika Halmashauri, atawajibika kufuata taratibu zote za Sheria Ndogo hii pamoja na Sheria nyingine zinazohusiana na ununuzi, uvunaji na usafirishaji wa mazo ya misitu.

SEHEMU YA SITA
USHURU WA MAZAO

Uwezo wa kutoza ushuru

10. (1) Halmashauri inaanzisha na kutoza ushuru wa mazao, kwa mazao yote yatakayozalishwa ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Ushuru huo utatozwa kutoka kwa kila mnunuzi kwa kiwango cha asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(3) Mnunuzi au mtu yeyote atakayesafirisha mazao yake ya chakula nje ya eneo la Halmashauri atalipa ushuru.

Wajibu wa Kujisajiri

11. (1) Kila mnunuzi wa mazao atatakiwa kujisajili kwa ajili ya kununua mazao ndani ya Halmashauri, na baada ya usajili atapewa kibali cha maandishi cha kununua mazao hayo.

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Kifungu cha (1) cha kifungu cha 11 hapo juu kitaonyesha;-

a) asili ya zao au mazao,
b) kiasi cha mazao,
c) kiasi cha ushuru utakaotozwa kwa ajili ya mazao yanayoombewa kibali,
d) eneo ambapo mazao hayo yatanunuliwa

Uwezo wa kuweka masharti

(3) Halmashauri inaweza kuongeza masharti yoyote kwenye kibali Kama itakavyoona inafaa, na mmiliki wa kibali hicho atatakiwa kufuata masharti hayo.

(4) Halmashauri inaweza kukataa kutoa kibali kwa mnunuzi yeyote ambaye anadaiwa ushuru wa mazao au kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hii.

Haki ya kukata kwa asiyeridhika na maamuzi

(5) Mnunuzi yeyote ambaye hataridhika na uamuzi utakaofanywa chini ya kifungu cha (4) atakata rufaa kwa Mkuu wa Mkoa ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(6) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi yeyote chini ya Sheria Ndogo hii;-

a) kununua au kusafirisha mazao bila kibali cha Halmashauri,
b) Kununua mazo shambani kabla ya kuvunwa,
c) kusafirisha mazao bila kulipa ushuru,
d) kununua mazao kwa kubadilishana na mali au nguo na kitu chochote kisichokuwa pesa
e) kununua mazao kwa njia ya kagomba, bata oil, kidochi na kipimo chochote kisichotambulika kisheria,
f) kununua mazao nje ya eneo lililotengwa kwa ajili ya kuuza na kununulia mazao.

(7) Mnunuzi yeyote atawajibika kutoa taarifa sahihi za mazao aliyonunua na kuonesha risiti aliyolipia ushuru pamoja na kibali cha kununulia mazao kwa Afisa muidhiniwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(8) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hii na utalipwa kabla ya mazao hayo hayajaondolewa kwenye eneo ambalo mazao hayo yamevunwa.

Uwezo wa kukamata na kushikilia mazao

(9) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata na kushikilia mazao yaliyonunuliwa kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii kwa siku saba (7)

Uwezo wa kuuza na kufidia gharama

(10) Baada ya siku saba (7) kupita na mmiliki hajakomboa mazao yake Halmashari itaomba kibali cha Mahakama na kuuza mazao hayo kwa njia mnada na kulipa fedha anazodaiwa na Halmashauri. Pia gharama za kukamata, gharama za ulinzi na uhifadhi wa mazao, zitakatwa kutoka kwenye mauzo hayo na salio atapewa mnunuzi.

Muda wa kusafirisha mazao

12. Ni marufuku kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusafirisha mazao kuanzia saa l:00 jioni hadi saa l2:00 asubuhi.

SEHEMU YA SABA
ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI VYA KIBIASHARA

13. (1) Kila wa chombo cha usafiri kama vile gari, pikipiki ya gurudumu mbili na pikipiki ya gurudumu tatu anayefanyia shughuli za biashara atapaswa kusajili chombo hicho Halmashauri kila mwaka. Ada ya usajili ni kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila chombo kitakachosajiliwa kitapatiwa cheti cha usajili pamoja na stika iliyotayarishwa na Halmashauri, stika hiyo itabandikwa sehemu inayoonekana ya kila chombo kama ushahidi wa malipo ya ada ya usajili.

(3) Ada ya usajili wa magari italipwa kabla ya tarehe 30 mwezi Juni, kila mwaka baada ya tarehe hiyo mmiliki atalipa ada anayodaiwa pamoja adhabu ya asilimia hamsini (50%) ya ada ya mwaka.

(4) Kila chombo kitapaswa kuegeshwa maeneo maalum yaliyoainishwa na Halmashauri. Itakuwa ni marufuku kwa chombo cha usafiri cha biashara kuegeshwa sehemu nyingine tofauti na eneo lililoainishwa.

SEHEMU YA NANE
USHURU WA MAEGESHO

14. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho wa magari kituoni kwa magari kama ifuatavyo hapa chini;-

a) kwa magari yatakayoegeshwa stendi,
b) kwa magari yanayotoka kituo kimoja na kupita eneo la stendi kuu kwenda sehemu nyingine,
c) kwa magari yanayoanzia stendi kuu ya magari.

(2) Ushuru huo utalipwa mara moja, siku ambayo atakwenda kulipa kwa viwango kama vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote;

a) kutengeneza au kuosha gari ndani ya stendi,
b) kuharibu miundombinu ndani ya stendi,
c) kupakia na kushusha abiria na mizigo nje ya eneo la stendi,
d) kutumia lugha ya matusi eneo la stendi.

SEHEMU YA TISA
USHURU WA MBAO ZA MATANGAZO

15. (1) Kila mfanyabiashara anayefanya biashara ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kuweka tangazo linalotambulisha biashara yake

(2) Tangazo hilo litabandikwa baada ya mfanyabiashara huyo kutuma maombi yaliyolipiwa ada kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi na kupata kibali kutoka kwa Halmashauri.

(3) Muda wa mwisho wa kulipa ushuru huo kwa hiari ni tarehe 30 Juni, ya kila mwaka na baada ya tarehe hiyo kupita ushuru huo utalipwa pamoja na faini ya asilimia hamsini (50%) ya ushuru.

(4) Matangazo yanayotolewa kwa mujibu wa masharti yaliyomo kwenye sheria ya Makampuni hayatatozwa ushuru.

Matangazo ya mdomo

(5) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote ndani ya eneo la Halmashauri kuzunguka na kipaza sauti na kutangaza tangazo lake bila kibali, isipokuwa kwa matangazo ya vifo au misiba.

(6) Mtu yeyote anayehitaji kutangaza tangazo lolote la kipaza sauti itabidi alipe ada ya matangazo ya kipaza sauti na kupatiwa kibali cha kutangaza.

SHEMU YA KUMI
USHURU WA MADINI YA UJENZI

16. (1) Halmashauri inaanzisha na kutoza ushuru wa madini ya ujenzi kutoka kwa kila mnunuzi wa madini hayo katika eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru huo utalipwa kwa Halmashauri au Wakala ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo kuthibitisha malipo hayo.

Tathimini ya athari kwa mazingira

17. Itakuwa ni wajibu wa kila mchimbaji wa madini ya ujenzi kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa mujibu wa sheria na kanuni za mazingira zilizopo hapa nchini kabla ya kuchimba madini hayo.

Kibali

18. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mchimbaji wa madini ya ujenzi kuwa na

kibali kabla hajaanza shughuli za uchimbaji katika eneo la Halmashauri. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuanza uchimbaji bila kuwa na kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Baada ya kufanya uchunguzi endapo uchimbaji huo hauna athari kwa mazingira na wakazi wa eneo yanapochimbwa madini hayo. Halmashauri itatoa kibali cha kuruhusu uchimbaji wa madini hayo kitakacholipiwa ushuru kwa kiwango kilichoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(3) Kibali kitakachotolewa na Halmashauri kitaeleza aina ya Madini yanayochimbwa na eneo yatakapochimbwa madini hayo.

Kuwasilisha taarifa za mapato

19. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika linalojishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi kutoa taarifa ya mapato yake ya mwaka au mwezi kama itakavyoelekezwa kwa Halamshauri.

Uwezo wa Afisa muidhiniwa

20. Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote zinapofanyika shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi wakati wa saa za kazi kwa lengo la kufanya ukaguzi na kukusanya takwimu sahihi za uchimbaji wa madini unaofanyika katika eneo hilo.

21. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au shirika kununua, kuuza, kutafiti, kuchimba au kusafirisha madini ya ujenzi bila kuwa na kibali cha Halmashauri.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI

Sheria Na. 16/2015

22. (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuanzisha na kutoza ushuru kwa kila mgeni atakayepanga chumba katika nyumba zote za wageni zilizoko ndani ya eneo la Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa.

(2) Ushuru utakaotozwa kutoka kwa wageni wanaopanga katika nyumba za wageni hautazidi kiasi cha asilimia kumi (10%) ya gharama za chumba kwa siku.

(3) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kupanga viwango kulingana na hali halisi ya mapato ya nyumba ya kulala wageni.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
USHURU WA MINARA

Ushuru wa minara

23. (1) Halmashauri itaanzisha na kutoza ushuru kwa minara yote iliyopo na itakayowekwa katika eneo lote lililopo chini ya mamlaka ya Halmashauri,

(2) Ushuru wa minara utalipwa Halmashauri kabla ya tarehe 30/09 kwa mwaka wa fedha uliopo kwa kiwango kama kilivyooneshwa

katika jedwali la Sheria ndogo hii.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
UTEUZI WA WAKALA

24. (1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kukusanya ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa niaba yake.

(2) Uteuzi unaofanywa chini ya kifungu cha (1) cha kifungu cha 24 hapo juu, unaweza kuwa kwa ajili ya eneo lote au sehemu ya eneo la Halmashauri au kwa ajili ya baadhi ya shughuli zinazolipiwa ada na ushuru.

Wajibu wa wakala

(3) Wakala atakayeteuliwa chini ya kifungu cha (1) cha kifungu cha 24 hapo juu, atawajibika:

a) kutoa taarifa ya maandishi juu ya majina au orodha ya watu au nyumba ambazo zinatakiwa au wanaotakiwa kutozwa ushuru au ada ndani ya eneo au sehemu ya eneo ambapo ameteuliwa kukusanya ushuru,
b) kukusanya na kupokea ada na ushuru kutoka kwa kila mtu anayedaiwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi,
c) kuwasilisha pesa zote alizokr-rsanya kwa Halmashauri,
d) kuwasilisha kwa Halmashari taarifa ya jina la mtu yeyote atakayeshindwa kulipa kiasi cha deni analodaiwa kwa ajili ya ada au ushuru wowote uliotozwa chini ya Sheria Ndogo hii.

SEHEMU YA KUMI NA NNE
MAKOSA NA ADHABU

Makosa

25. (1) (i) Wakala yeyote aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi:-

a) atakayeshindwa kuwasilisha Halmashauri kiasi chochote cha pesa za ada au ushuru alizokusanya, au
b) ambaye kwa kufahamu atamtoza mtu yeyote kiasi cha ada au ushuru zaidi ya kile kilichowekwa chini ya Sheria Ndogo hizi; au
c) ambaye kwa uzembe au kwa kufahamu atatoa taarifa za uongo kwa mdomo au kwa maandishi juu ya idadi ya walipa ushuru au kiasi cha ada au ushuru alichokusanya au alichopokea au
d) ambaye kwa makusudi atashindwa kutekeleza wajibu kama wakala chini ya kifungu cha 25 cha Sheria ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(ii) Mtu yeyote ambaye;-

a) atakataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru,
b) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe ushuru,
c) atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake,
d) atajenga jengo lolote bila kuwa na kibali cha ujenzi,
e) atachinja mifugo bila kukaguliwa, au
f) atatenda kitendo chochote ambacho kinaonekana kinaweza kuathiri mapato au ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.

Adhabu

(2) Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, iwapo atashitakiwa mahakamani na kupatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu (Tshs 300,000/=) au kutumikia kifungo gerezani kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Mkosaji kufidia gharamia alizosababisha

(3) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika Sheria Ndogo hizi, mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

26. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini ya kiasi cha pesa anachodaiwa baada ya mtu huyo kukiri kosa kwa maandishi kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika jedwali 1a pili la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

(A) Ushuru wa machinjio na ukaguzi wa nyama

(i) Ushuru wa machinjio

a)	Ng'ombe	Tshs	10,000/=
b)	Mbuzi & kondoo	Tshs	5,000/=
c)	Nguruwe	Tshs	5,000/=

(ii) Ushuru wa ukaguzi wa mnyama na nyama

d)	Ng'ombe	Tshs	1,500/=
e)	Mbuzi & kondoo	Tshs	800/=
f)	Nguruwe	Tshs	800/=

(B) Ada ya pango la nyumba na vibanda vya Halmashauri.

(i) Pango la nyumba kwa watumishi wa Halmashauri Tshs 20,000/= kwa mwezi,

(ii) Pango kwa wapangaji wasio watumishi wa Halmashauri itatajwa kwenye mkataba baina ya wapangaji hao na Halmashauri.

(iii) Ada ya pango kwa vibanda:

a) Vibanda vya maduka ndani na nje ya soko Tshs 25,000/=

b) Vibanda vya maduka ndani\ nje ya stendi Tshs 25,000/=

MUHIMU; Pango ya vibanda hivi italipwa kwa mwezi

(C) Ushuru wa Mazao

(i) Ada ya maombi ya kununua mazo ya biashara Tshs 600,000/=

(ii) Ada ya maombi ya kununua mazao ya chakula Tshs 450,000/=

MUHIMU: Ada itabadilika kulingana na mahitaji ya wakati

(iii) Ushuru wa mazao

a)	Korosho	5% ya bei ya kununulia
b)	Mahindi	5% ya bei ya kununulia
c)	Ufuta	5% ya bei ya kununulia
d)	Mbaazi	5% ya bei ya kununulia
e)	Kunde	5% ya bei ya kununulia
f)	Vitunguu	5% ya bei ya kununulia
g)	Mtama	5% ya bei ya kununulia
h)	Mihogo	5% ya bei ya kununulia
i)	Choroko	5% ya bei ya kununulia
j)	Karanga	5% ya bei ya kununulia
k)	Mpunga	5% ya bei ya kununulia
l)	Njungu	5% ya bei ya kununulia
m)	Nyanya	5% ya bei ya kununulia
n)	Nazi	5% ya bei ya kununulia

(D) Ada ya usajiri wa vyombo vya usafiri vya kibiashara

Aina ya Chombo		**Kiwango**		**Muda**
i)	Basi la abiria I -25	Tshs	20,000/=	kwa mwaka
ii)	Basi la abiia 26-45	Tshs	35,000/=	kwa mwaka
(iii)	Basi la abiria 46- 65	Tshs	75,000/=	kwa mwaka
(iv)	Zaidi abiria 65	Tshs	90,000/=	kwa mwaka
(v)	Taxi	Tshs	30,000/=	kwa mwaka
(vi)	Lori chini ya tani 7	Tshs	40,000/=	kwa mwaka
(vii)	Lori zaidi ya tan 7	Tshs	50,000/=	kwa mwaka
(viii)	Pikipiki	Tshs	15,000/=	kwa mwaka
(viii)	Pikipiki ya gurudumu tatu	Tshs	25,000/=	kwa mwaka

(E) Ada na Ushuru wa Mazao ya Misitu

NA	AINA YA ZAO	KIPIMO/KIASI	USHURU Tshs
1	Mkaa	Gunia moja	1,000/=
2	Ubao	mmoja	1,000/=
3	Shata mlango/dirisha	Moja	4,000/=
4	Fremu mlango/dirisha	Moja	2,500/=
5	Kitanda	Kimoja	5,000/=
6	Kabati	Moja	5,000/=
7	Kochi	Moja	1,500/=

8	Vikapu	Kwa kilo moja	100/=
9	Vinyago vya mpingo	Kwa kila kilo moja	250/=
10	Vinyango vya miti mingine	Kwa kila kilo moja	150/=
10	Viti, Stuli, Vitu vidogovidogo	Kwa kila kimoja	750/=
11	Kuni	$1m^3$	250/=
12	Nguzo(Kipenyo 5sm-10sm)	Mmoja	70/=
13	Nguzo (Kipenyo 11sm-20sm)	Mmoja	100/=
14	Mwanzi (Kipenyo > 5sm)	Mmoja	100/=
15	Mwanzi (Kipenyo < 5sm)	Mmoja	100/=
16	Gundi	Kwa kilo	40/=
17	Dawa ya mitishamba majani	Kwa kilo	20/=
18	Dawa za mitishamba mizizi	Kwa kilo	40/=
19	Asali	Kwa kilo	100/=

(F) Ada ya Shughuli za kiutamaduni

(i) Ada ya kusajili kikundi cha Sanaa/muziki Tshs 20,000/= kwa mwaka

(ii) Ada ya kibali disko au muziki
a) Kikundi ndani ya wilaya Tshs 30,000/= kwa kila onesho
b) Kikundi toka nje wilaya Tshs 50,000/= kwa kila onesho
c) Kikundi toka nje ya Mkoa Tshs 100,000/= kwa kila onesho

(ix) Ada ya kibali cha kuonesha sanaa za maonesho, maigizo, sarakasi, ngumi au mieleka, kunyanyua vyuma na mazingaombwe Tshs 10,000/= kwa kila onesho
(x) Ada ya kibali cha kuonesha sinema kwa malipo kwa mwezi 30,000/=
(xi) Ada ya kufanya shughuli za kimila (unyago) Tshs 20,000/= kwa kila shughuli

(G) Ushuru wa soko
a) Kupanga meza ndani ya soko Tshs 1,000/= kwa siku
b) Kupanga kizimba katika soko Tshs 1,000/= kwa siku

(H) Ada ya Ukaguzi wa Afya

(a) kupima afya za wahudumu wa hoteli, migahawa Tshs 10,000/= kila mmoja
(b) kupima afya kwa baba au mama lishe Tshs 10,000/= kila mmoja
(c) kutumia choo cha umma Tshs 300/= kwa mtumiaji mmoja kwa mara moja.

(I) Ushuru wa Mbao za Matangazo

(a) **Mabango yanaotoa Mwanga** (illuminated)

(i) Ada ya kibali cha kuweka bango Tshs 20,000/= kwa mwaka,

(ii) Bango lenye ukubwa wa futi moja ya mraba Tshs 20,000/= kwa mwaka

(iii) Bango linalozidi ukubwa wa futi moja ya mraba Tshs 5,000/= kwa kila futi inayoongezeka kwa mwaka,

(b) **Mabango yasiyotoa Mwanga (non-illurninated**)

(i) Ada ya kibali cha kuweka bango Tshs 20,000/=

(ii) Bango lenye ukubwa wa futi moja ya mraba Tshs 20,000/= kwa kila bango kwa mwaka,

(iii) Bango linalozidi ukubwa wa futi moja ya mraba Tshs 2,000/= kwa kila futi inayoongezeka kwa mwaka,

(iv) Ushuru wa matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti Tshs 5,000/= kwa siku, kwa tangazo.

(J) ADA YA VIBALI VYA UJENZI

a) maeneo yenye ujazo mdogo wa watu Tshs 100,000/=
b) maeneo yenye ujazo wa kati wa watu Tshs 75,000=
c) maeneo yenye ujazo wa juu wa watu Tshs 50,000/=
d) kubadili matumizi ya ardhi, kwa kiwanja kimoja Tshs 150,000/=
e) kugawanya kiwanja, kwa kiwanja Tshs 150,000/=
f) kuhakiki miliki Tshs 30,000/=
g) kuzingira maeneo ya ghorofa, kwa mwaka Tshs 50,000/=

(K) USHURU WA MADINI YA UJENZI

(1) Ada ya kibali kwa Uchimbaji Tshs 100,000/= kwa mwaka

(2) Viwango vya Ushuru

a) Mchanga M^3 tatu na nusu (3.5) Tshs 2,500/=
b) Mchanga ghafi M^3 moja (1) Tshs 10,000/=
c) Kokoto M^3 tatu na nusu (3.5) Tshs 2,500/=

d) Mawe M^3 tatu na nusu (3.5) Tshs 2,500/=
e) Mawe ya mapambo M^3 moja (1) Tshs 10,000/=
f) Kifusi M^3 tatu na nusu (3.5) Tshs 2,500/=

(L) USHURU WA MINARA YA SIMU

Minara ya Mawasiliano ……. Kwa mwaka ……Tshs 1,000,000/= kwa mnara mmoja.

(M) USHURU WA MAEGESHO STENDI

a) Magari makubwa Tshs 2,000/=
b) Magari madogo Tshs 1,000/=
c) Pikipiki / Bajaji Tshs Tshs 500/=

JEDWALI LA PILI
SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA
(AADA NA USHURU) MWAKA 2015

HATI YA KUKIRIKOSA
(chini ya kifungu cha 26 ya Sheria ndogo hizi)

Mimi …….. Nakiri mbele ya ……., Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa kwamba mnamo tarehe…… mwezi …… mwaka ……. nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa (Ada na Ushuru) za Mwaka 2015. Nipo tayari kulipa kiasi cha Ada/Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini, ikiwa Mkurugenzi ataamua kuutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya Sheria Ndogo hii kama ilivyotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari na ufahamu wangu.

Tarehe ……..

Saini ……

Nembo ya Halmashauri imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 01 Mwezi 07 Mwaka 2016 na umebandikwa mbele ya:-

ANDREA G. CHEZUE
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

RASHIDI NAKUMBYA
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

NAKUBALI

George B. Simbachawene (Mb)
WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI

DODOMA ……